

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI IFAKARA



01/11/2022

TANGAZO

TAARIFA KUHUSU UTARATIBU WA WA KUWAREJESHEA MICHANGO
YA WAFANYAKAZI 05% PSSSF AU 10% NSSF KWENYE MIFUKO YA
HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WALIOFUKUZWA KAZI KWA KOSA
LA KUGHUSHI VYETI 2016/2017

Kufuatia maelekezo kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Raisi menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa Waraka wenye Kumb.Na. CFC.26/205/01"AT"/20 wa tarehe 31 Oktoba, 2022 kuhusu utaratibu tajwa hapo juu.

Mkurugenzi wa Mji Ifakara anawatangazia waliokuwa Watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara na kufukuzwa kazi kwa Kughushi Vyeti kufika katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji wa Ifakara kwa ajili ya kukamilisha taratibu za malipo ya michango iliyowasilishwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii katika kipindi walichokuwa Watumishi wa Umma kabla ya kuondolewa.

Watumishi hao wanatakiwa kufika na nyaraka zifuatazo;-

- i. Picha mbili za ukubwa wa Passport size.
- ii. Nakala ya taarifa za Benki (Bank statement) ya Akaunti iliyohai.
- iii. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa au Mpiga kura au Leseni ya udereva.

Kwa mawasiliano zaidi.

Oscar P. Simtengu

Kny: MKURUGENZI WA MJI IFAKARA.



Wasiliana na dawati la msaada kwa namba;-

Oscar Simtengu; TAHRO – 0784241146

Sairis Mbiro: HRO - 0714200458